



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS
TAMKO LA WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO
NA MAZINGIRA), MHE. MHANDISI. HAMAD YUSSUF MASAUNI (MB.)
KUHUSU TANZANIA
MWENYEJI WA MKUTANO WA 12 WA NCHI WANACHAMA WA
MKATABA WA NAIROBI (COP12),UTAKAOFANYIKA
DAR ES SALAAM TAREHE 06-09 OKTOBA 2026

Ndugu Wanahabari ,

Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutujalia uzima na afya njema, na kutuwezesha kukusanyika hapa siku ya leo.

Pia, ningependa kuwashukuru wote kwa kutenga muda wenu kuja kuungana nasi katika siku hii ya leo. Hii inadhihirisha utayari wa kuendeleza jukumu la kuhifadhi rasilimali ya Bahari ya Hindi kwa maendeleo endelevu nchini.

Ndugu Wanahabari,

Kwa namna ya kipekee, napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri hususan katika kuipa kipaumbele Sekta ya Mazingira na uhifadhi wa rasilimali za bahari.

Dhamira hiyo imeonekana kupitia hatua za Serikali za kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa rasilimali maji za Bahari, Mito, Maziwa, maji chini ya ardhi na maeneo oevu.

Kutokana na umuhimu huo Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeanzisha Kitengo mahsusi cha kuratibu maendeleo ya Uchumi wa Buluu ambayo inahusisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari kwa ajili ya kukuza uchumi na ustawi wa jamii.

Ndugu Wanahabari,

Kama tunavyoendelea kupata taarifa kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea na maandalizi ya Mkutano wa 12 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Nairobi (COP12), utakaoanza tarehe 06 hadi 09 Oktoba, 2026 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere, Jijini Dar es Salaam (JNICC).

Kwa mwaka 2026 Mkutano wa COP12 utafanyika jijini Dar es Salaam nchini Tanzania huku ukichagizwa na **Kaulimbiu ya kitaifa ambayo ni: “Towards a Sustainable Blue Economy in the Western Indian Ocean for People and Nature: A 40 - Year Journey”** ambapo kwa lugha ya Kiswahili inamaanisha **“Kuelekea Uchumi wa Buluu Endelevu katika Ukanda wa Magharibi wa Bahari ya Hindi kwa Manufaa ya Watu na Mazingira ya asili: Safari ya Miaka 40.**

Ndugu Wanahabari,

Miongoni mwa **Mambo makuu yatakayojadiliwa katika mkutano huo ni pamoja na:** Kudhibiti uchafuzi wa bahari na pwani, ikiwemo uchafuzi unaotokana na shughuli za nchi kavu na shughuli za baharini; Kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira ya bahari, ikiwemo rasilimali na mifumo ya ikolojia inayovuka mipaka; Kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuongeza ustahimilivu wa jamii, miundombinu na mifumo ya ikolojia ya pwani. Mkutano huo pia utajadili uhifadhi wa bioanuai ya bahari na pwani, ikiwemo mikoko, matumbawe, nyasi bahari na maeneo muhimu ya ikolojia; Kuendeleza Uchumi wa Buluu endelevu, kwa kuunganisha uhifadhi wa mazingira na uwekezaji, biashara, ajira na maendeleo ya jamii za pwani; Kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika usimamizi wa rasilimali zinazovuka mipaka, ikiwemo uvuvi, maeneo ya hifadhi na rasilimali za bahari; Kuimarisha ushirikiano wa kisayansi, teknolojia na Marine Spatial Planning (MSP) katika kufanya maamuzi yanayozingatia taarifa na ushahidi wa kisayansi na kujenga misimamo ya pamoja katika masuala ya kimataifa kama Biodiversity Beyond National Jurisdiction-BBNJ, yaani uhifadhi na matumizi endelevu ya anuwai ya kibiolojia ya bahari katika maeneo yaliyo nje ya mamlaka ya kitaifa na utawala wa bahari.

Sambamba na hayo, COP12 itajadili na kupitisha **maamuzi ya Mkutano wa Nchi Wanachama**, pamoja na **Joint Ministerial Declaration**, na kufanya **uchaguzi wa baraza la viongozi** kwa kipindi 2026/2028.

Ndugu Wanahabari

Kutokana na Tanzania kupata heshima ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa COP12, inayo matarajio mengi ambayo ni kuimarisha diplomasia ya Mazingira ya Tanzania na kuongeza ushawishi wake katika masuala ya Mazingira ya bahari na pwani katika ngazi ya kikanda na Kimataifa; kupata maazimio na hatua za pamoja za kulinda bahari, uvuvi haramu, uharibifu wa mifumo ikolijia na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mkutano huo utaweza kutoa Azimio La DSM; kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika Uchumi wa Buluu ili kuongeza fursa za uvuvi endelevu, aquaculture, utalii wa baharini, usafiri wa majini na uwekezaji unaozingatia mazingira; kuvutia fedha, teknolojia uwekezaji unaozingatia mazingira; kuvutia fedha, teknolojia na uwekezaji kwa ajili ya uhifadhi wa bahari ya Pwani, Mabadiliko ya tabianchi, udhibiti wa uchafuzi na miradi ya Uchumi wa Buluu; kuimarisha uhifadhi wa Bionuai ya bahari ya Pwani, ikiwemo mikoko, matumbawe, nyasi bahari na maeneo muhimu ya mazalia ya viumbe baharini; kukuza manufaa kwa jamii za Pwani, kupitia ajira, uvuvi endelevu, aquaculture, uhifadhi shirikishi na fursa nyingine za Uchumi wa Buluu kuimarisha utekelezaji wa Mikataba na mifumo ya Kimataifa, ikiwemo Nairobi Convention, United Nations Conventions on the Law of the Sea (UNCLOS); Biodiversity Beyond National Jurisdiction Agreement (BBNJ Agreement); Convention Of Biodiversity (CBD); United Nations Framework Convention On Climate Change (UNFCCC) na International Convention for the Prevention of Pollution from Ships (MARPOL)

Ndugu Wanahabari,

Wahenga walinena mgeni njoo mwenyeji apone, ndivyo usemi huu unavyojidhihirisha kwakuwa ni dhahiri mkutano huu unatarajiwa kuleta fursa kwa wananchi na Taifa kwa ujumla. Mkutano huu utaweza kuvutia uwekezaji katika Uchumi wa Buluu, kuunganisha wawekezaji na fursa za uwekezaji katika uvuvi, utalii wa baharini, kilimo cha mwani, bioeconomy na huduma za ikolojia; Kuchochea upatikanaji wa fedha za mazingira na tabianchi; Kuunganisha Tanzania na mifuko ya kimataifa na taasisi za fedha kwa ajili ya miradi ya uhifadhi wa bahari na pwani, mabadiliko ya tabianchi, uchafuzi na bioanuwai; Kuimarisha utekelezaji wa Marine Spatial Planning (MSP) na Kutumia COP12 kupata utaalamu, teknolojia na ushirikiano wa kikanda katika kupanga matumizi endelevu ya maeneo ya bahari.

Ndugu Wanahabari,

Lengo la Serikali ni kuhakikisha fursa za Uchumi wa Buluu zinawafikia wananchi, hususan jamii zinazotegemea bahari na pwani. Manufaa yanayopatikana kupitia sekta hii ni pamoja na ajira, uvuvi endelevu, ufugaji viumbe maji, utalii, biashara, huduma na kuongeza thamani ya mazao.

Pamoja na mambo mengine, kupitia utekelezaji wa Mkataba wa Nairobi, jamii zinazotegemea rasilimali za bahari na pwani zimepata manufaa mbalimbali, yakiwemo; Kuongezeka kwa uelewa wa jamii kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali za bahari na pwani, hususan kupitia elimu na ushirikishwaji wa wananchi katika usimamizi wa maeneo ya bahari; Kuimarika kwa shughuli za kujipatia kipato na maisha ya jamii za wavuvi, kupitia utekelezaji wa miradi inayolenga usimamizi endelevu wa uvuvi na rasilimali za bahari, hususan katika maeneo ya Mkinga na PECCA; Kushirikishwa kwa jamii katika urejeshaji na uhifadhi wa misitu ya mikoko, ikiwemo katika Delta ya Rufiji, jambo linalosaidia kulinda maeneo ya mazalia ya samaki, kupunguza mmomonyoko wa fukwe na kuhifadhi rasilimali zinazotegemewa na jamii na Kuimarika kwa mazingira ya bahari na pwani kutokana na kupunguza uchafuzi, kupitia miradi ya usimamizi wa taka za plastiki, maji machafu na vyanzo vingine vya uchafuzi vinavyoingia baharini.

Ndugu Wanahabari,

Manufaa mengine ni pamoja na Kuboresha huduma za usafi wa mazingira kwa jamii, kupitia ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya ukusanyaji na usafishaji wa maji machafu, ikiwemo katika eneo la Chake Chake, Pemba; Kuongezeka kwa ushiriki wa wanawake katika shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira, ikiwemo kupitia mafunzo na shughuli za urejeshaji wa mazingira katika maeneo ya jamii na Kuongezeka kwa uwezo wa jamii katika usimamizi wa rasilimali za maji na mazingira, kupitia mafunzo na ushirikishwaji katika usimamizi wa mito, mabonde na maeneo ya pwani.

Kupitia Uchumi wa Buluu wananchi wa jamii ya pwani wananufaika kwa Kulindwa na kurejeshwa kwa mifumo muhimu ya ikolojia, ikiwemo mikoko, matumbawe, nyasi bahari na maeneo mengine ya asili ambayo ni muhimu kwa uvuvi, kinga ya fukwe na ustawi wa jamii; Kupunguza athari za mmomonyoko wa fukwe na uharibifu wa maeneo ya pwani, kupitia urejeshaji wa uoto wa asili na hatua nyingine za kulinda maeneo yaliyo hatarini na Kuongezeka kwa fursa za wananchi kushiriki katika Uchumi wa Buluu, kutokana na kuimarishwa kwa usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari na pwani, hivyo kuweka mazingira bora kwa

shughuli za uvuvi, aquaculture na shughuli nyingine za kiuchumi zinazotegemea bahari.

Ndugu Wanahabari,

Wakati nikihitimisha taarifa hii, ningependa kusema matarajio ya Tanzania ni kuhakikisha Mkutano wa COP12 unaleta matokeo yanayolinda mazingira ya bahari na pwani, yanaimarisha Uchumi wa Buluu, yanaongeza ushirikiano wa kikanda na kimataifa, na hatimaye kuleta manufaa kwa wananchi, hususan jamii zinazotegemea rasilimali za bahari na pwani.

Hivyo, nitoe wito kwa wadau wote Wizara, Taasisi za Umma, Sekta Binafsi, Wanazuoni, Watafiti, Mashirika ya Kiraia na Wananchi kwa ujumla – kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya mkutano huu. Ushiriki wenu utaimarisha mafanikio ya mkutano na kuongeza tija kwa Taifa letu.

Kwa pamoja, tuendeleo kulinda na kuhifadhi rasilimali zetu za bahari na pwani kwa ustawi wa kizazi cha sasa na kijacho kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu.

Nashukuru kwa kunisikiliza!

**MHE. MHANDISI HAMAD M.Y MASAUNI
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA)**